Thamani ya Roho

na

Ellis Forsman

Thamani ya Roho

na

Ellis Forsman

Oktoba 15, 2011

Thamani Ya Roho

Mat. 16:26

Mat. 16:26, "*Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote na kupata hasara ya nafsi yake? Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake?*"

Mambo mawili yanaonekana katika maswali haya mawili ambayo Kristo anauliza:

Kwamba ni hao wanao jitahidi kuupata ulimwengu, na hawapendi kuiacha kwa sababu ya nafsi, watapoteza nafsi yake.

Kwamba kama nafsi itapotea, hakuna kitu kitakachotolewa mbadala, kwa sababu haiwezi kuokolewa vile vile. Hakuna ukombozi motoni.

Mara nyingi tunajali mambo ya kimwili, lakini mara nyingi tunaonyesha mvuto kidogo kwenye mambo ya kiroho.

Tuna vitu vyetu na hata maisha yetu yamehakikishwa.

Tunaweka pesa kwenye benki, na kuwa na ulinzi mwingine.

Wakati miili yetu ya damu na nyama na vitu tunavyomiliki viko katika hatari ya kuungua moto ndani ya nyumba, tunajaribu kujiokoa sisi wenyewe na kifaa cho chote tunachoweza kubeba. Lakini, vipi kuhusu nafsi zetu? Iko katika hatari ya kuungua moto. Je! Haipaswi kuwa mhimu, au zaidi?

Nafsi: Ni nini?

Roho.

Mhu. 12:7, "*Nayo mavumbi kuirudia nchi kama yalivyokuwa, nayo roho kumrudia Mungu aliyeitoa.*"

Ni kati ya mwanadamu anachokipenda, chukia, tarajia, omba, amini, panda, kujaribiwa, dhambi, tubu, na atakuwa ameokolewa milele au kupotea.

Thamani yake ni nini? Thamani yake inaonekana katika:

Kwamba inathamani kuliko ulimwengu.

Mat. 16:26, "*Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote na kupata hasara ya nafsi yake? Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake?*"

Kwamba inathamani kuliko mwili.

- 2 Kor. 4:16, "*Kwa hiyo hatulegei bali ijapokuwa utu wetu wa nje unachakaa, lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku.*"
- 2 Kor. 5:1, "*Kwa maana twajua ya kuwa nyumba ya maskani yetu iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tunalo jengo litokalo kwa Mungu, nyumba isiyofanywa kwa mikono, iliyo ya milele mbinguni.*"

Kwamba haufi.

1 Kor. 15:54, "*Basi huu uharibikao utakapovaa kutokuharibika, na huu wa kufa utakapovaa kutokufa, hapo ndipo litakapokuwa lile neno lililoandikwa, mauti imemezwa na kushinda.*"

Kwamba mwanadamu hawezi kuuangamiza.

Mat. 10:28, "*Msiwaogope wauao mwili, wasiweze kuiua na roho; afadhali mwogopeni yule awezaye kuangamiza mwili na roho pia katika jehanum.*"

Kwamba lazima irudi kwa Mungu.

Mhu. 12:7, "*Nayo mavumbi kuirudia nchi kama yalivyokuwa, nayo roho kumrudia Mungu aliyeitoa.*"

Kwamba itatumia umilele katika moja ya sehemu mbili.

- Mat. 7:13-14, "*Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba, maana mlango ni mpana na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache.*"
- Mat. 25:46, "*Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele.*"

Majukumu ya nafsi:

Kupenda. Mat. 22:37, "*Akamwambia mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote.*"

Kufikiri. Mith. 23:7, "*Maana aonavyo nafsini mwake, ndivyo alivyo. Akuambia haya kula, kunywa; lakini moyo wake hauwi pamoja nawe.*"

Kutii. Rum. 6:17, "*Lakini Mungu na ashukuriwe, kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake.*"

Gharama iliyolipiwa.

1 Petr. 1:18-19, "*Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo*

wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo."

Haiwezi kurudishwa kama ikipotea.

Mungu amempa kila mtu nafsi moja na moja pekee; kama ikipotea, vyote vimepotea.

Unaweka thamani gani katika nafsi yako?

Unasemaje kuhusu matendo yako yanayoonyesha ni kitu gani nafsi yako ina uthamani gani?

Wote tutasema kwamba haina thamani yo yote tunapokuwa katika mdahalo, Lakini katika mienendo ya maisha yetu je tunaonyesha tunachokithamini au nafsi?

Badala yake, je tunaonyesha kwamba tunaupenda ulimwengu kuliko upendo wa Mungu?

Watu wengine wanatenda kana kwamba nafsi zao zina thamani ndogo, kwa sababu hawajali na hawajali kuhusu hali ya nafsi zao.

Dunia

Ni nini?

- 1 Yoh. 2:15-16, "*Msiipende dunia wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake. Maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia.*"
- Mhu. 2:1, "*Nikauambia moyo wangu, haya nitakujaribu kwa njia ya furaha basi ujifurahishe kwa anasa. Na tazama hayo nayo yakawa ubatili.*"
- Mhu. 5;10, "*Apendaye fedha hatashiba fedha, wala apendaye wingi hatashiba nyongeza. Hayo pia ni ubatili.*"
- 1 Tim. 6:10, "*Maana shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha; ambayo wengine hali wakiitamani hiyo wamefarakana na imani, na kujichoma kwa maumivu mengi.*"

Faida yako itakuwa nini kama ukipata ulimwengu?

Kitu ambacho hakiwezi kuridhisha.

- Yoh. 4:13-14, "*Yesu akajibu akamwambia kila anywaye maji haya ataona kiu tena; walakini ye yote atakayekunywa maji yale nitakayompa mimi hataona kiu milele; bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele.*"

- Mat. 4:4, "*Naye akajibu akasema imeandikwa mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.*"

Kitu ambacho kinaharibika.

1 Yoh. 2:17, "*Na dunia inapita pamoja na tamaa zake, bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata milele.*"

Kitu ambacho lazima kiachwe katika ulimwengu huu.

- Luka 12:16-21, "*Akawaambia mithali akisema lamba la mtu mmoja tajiri lilikuwa limezaa sana; akaanza kuwaza moyoni mwake akisema, nifanyeje? Maana sina pa kuyaweka akiba mavuno yangu. Akasema nitafanya hivi; nitazivunja ghala zangu nijenge nyingine kubwa zaidi, na humo nitaweka nafaka yangu yote na vitu vyangu. Kisha nitajiambia ee nafsi yangu una vitu vyema vingi ulivyojiwekea akiba kwa miaka mingi; pumzika basi, ule, unywe, ufurahi. Lakini Mungu akamwambia, mpumbavu wewe, usiku huu wa leo wanataka roho yako! Na vitu ulivyojiwekea tayari vitakuwa vya nani? Ndivyo alivyo mtu ajiwekeaye nafsi yake akiba, asijitajirishe kwa Mungu.*"

- 1 Tim. 6:6-8, "*Walakini utauwa pamoja na kuridhika ni faida kubwa. Kwa maana hatukuja na kitu duniani, tena hatuwezi kutoka na kitu; ila tukiwa na chakula na nguo tutaridhika na vitu hivyo.*"

Hasara yako itakuwa nini kama ukiupata ulimwengu?

Ulimwengu.

Kile ambacho umepata kwa thamani kubwa kitapotea, kwa maana nafsi iliyopotea haiwezi kuchukua ulimwengu huu pamoja naye hadi katika ulimwengu mwingine.

Vile vile, mwanadamu anayepoteza nafsi yake kwa kupata pesa, sio tu kwamba anapoteza nafsi yake, bali hata pesa pia.

Yule anayepata heshima ya kibinadamu kwa gharama ya nafsi yake atazipoteza, maana hazitakuwa na thamani kwake motoni.

Hivyo basi, nafsi inapotea kwa faida ya ulimwengu haimanishi kwamba ulimwengu umepatwa, maana hawezi kuchukua kile alichokipata katika ulimwengu huu hadi katika ulimwengu ujao.

Muda wa maisha ya utumishi.

Maisha ya miaka mingi ambayo ingeweza kutolewa kwa utukufu wa Mungu na huduma vyote vimepotea.

Mat. 25:14-30, "*Maana ni mfano wa mtu atakaye kusafiri, aliwaita watumwa wake, akaweka kwao mali zake. Akampa mmoja talanta tano, na mmoja talanta mbili, na mmoja talanta moja; kila mtu kwa kadiri ya uwezo wake; akasafiri. Mara yule aliyepokea talanta tano akaenda, akafanya biashara nazo, akachuma faida talanta nyingine tano. Vile vile na yule mwenye mbili, yeye naye akachuma nyingine mbili faida. Lakini yule aliyepokea moja alikwenda akafukua chini akaificha fedha ya bwana wake. Baada ya siku nyingi akaja bwana wa watumwa wale, akafanya hesabu nao. Akaja yule aliyepokea talanta tano, akisema Bwana, uliweka kwangu talanta tano; tazama talanta nyingine tano nilizopata faida. Bwana wake akamwambia vema mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi ingia katika furaha ya bwana wako. Akaja yule aliyepokea talanta mbili akasema, Bwana, uliweka kwangu talanta mbili; tazama talanta nyingine mbili nilizopata faida. Bwana wake akamwambia vema mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako. Akaja na yule aliyepokea talanta moja, akasema Bwana nalitambua ya kuwa wewe u mtu mgumu, wavuna usipopanda, wakusanya usipotawanya; basi nikaogopa nikaenda nikaificha talanta yako katika ardhi tazama unayo iliyo yako. Bwana wake akajibu akamwambia, wewe mtumwa mbaya na mlegevu ulijua ya kuwa navuna nisipopanda, nakusanya nisipotawanya; basi ilikupasa kuweka fedha yangu kwa watoa riba, nami nikija ningalipata iliyo yangu na faida yake. Basi mnyang'anyeni talanta hiyo, mpeni yule aliye nazo talanta kumi. Kwa maana kila mwenye kitu atapewa, na kuongezewa tele; lakini asiye na kitu, hata kile alicho nacho atanyang'anywa. Na mtumwa yule asiyefaa, mtupeni mbali katika giza la nje; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno.*"

Nafsi iliyopotea haiwezi kuponyeshwa - imepotea milele.

Kama ukiipoteza nafsi yako katika hali ya raha, utajiri, heshima, umaarufu, nk., hautaweza umilele yote kuwa na nafasi ya kukomboa hasara.

Imepotea Motoni.

- Rum. 6:23, "*Maana mshahara wa dhambi ni mauti bali karama ya Mungu ni uzima wa milele kupitia Yesu Kristo Bwana wetu.*"

- Luka 16:26, "*Na zaidi ya hayo kati yetu sisi na ninyi kumewekwa shimo kubwa, ili wale watakao kutoka huku kwenda kwenu wasiweze; wala watu wa kwenu wasivuke kuja kwetu.*"

Tajiri alijifunza somo lake akiwa amechelewa sana.

Katika kifo alijifunza somo ambalo lingefaa ajifunze katika maisha.

Ezek. 18:20-21, "*Roho itendayo dhambi ndiyo itakayokufa; mwana hatauchukua uovu wa baba yake, wala baba hatauchukua uovu wa mwanawe, haki yake mwenye haki itakuwa juu yake, na uovu wake mwenye uovu utakuwa juu yake. Lakini mtu mbaya akighairi, na kuacha dhambi zake zote alizozitenda na kuzishika amri zangu zote, na kutenda yaliyo halali na haki, hakika ataishi hatakufa.*"

Hitimisho

Nafsi iliyopotea ni uvunjifu mkubwa na uharibifu unaowezekana, wakati nafsi iliyookolewa ni ukamilifu mkuu na mafanikio yanayowezekana.

Chaguo lako litakuwa nini?

- Wokovu wa milele kupitia kutii kwako injili, au:
- Maangamizi ya milele.

Pima madhara na uchague sasa.

Ebr. 3:7-8, "*Kwa hiyo kama anenavyo Roho Mtakatifu, leo kama mtaisikia sauti yake, msifanye migumu mioyo yenu,…*"

Mtu anawezaje kufanyika Mkristo? Zifuatazo ni hatua muhimu kufanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Ebr. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza, kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*" Nilipokuwa katika kidato cha tano na sita (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na wangu, akaniambia kwamba haamini kwamba Mungu yuko. Kwa vile nilikuwa nimeshabatizwa nilichukua nafasi ya kuongea naye kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya Ukristo ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamba anaamini kwamba kuna Mungu. Lakini ili awe sehemu salama, labda anapaswa kwenda kanisani, na siku akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kwamba anakwenda

kanisani na kuishi maisha mazuri kwamba Mungu atamruhusu kuingia mbinguni (kama kuna mbingu), na sio motoni (kama kuna moto). Nikamwambia "Hayaendi hivyo. Unapaswa umwamini kwa moyo wako wote bila hivyo huwezi kumpendeza."

- **Toba.** Mdo. 2:38, "*Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" Mdo. 11:18, "*…Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima.*" Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba nyingine, na ukajifikiria mwenyewe, "Kuna mwizi ndani ya nyumba yangu!" hivyo unachukua simu taratibu, na kuwapigia polisi, ukiwaambia kuna mwizi ndani ya nyumba yako, unawapa anuani ya nyumba yako. Muda mfupi unawasikia wamefika na kumkamata mwizi. Anapiga kelele, "Samahani; Samahani!" Anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu ameshikwa; sio kwamba alikuwa anaiba. Katika toba ya kweli mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba na kwamba anataka kubadili maisha yake ili kwamba asiibe tena. Hiyo ndio toba ya kweli. Ni badiliko la nia linalo sababisha badiliko la tendo. Hicho ndicho tunatakiwa kufanya kabla hatujafanyika Wakristo.

- **Kukiri.** Rum. 10:9-10, "*Ukimkiri Yesu kwa kinywa chako kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni wako kwamba Mungu alimfufua katika wafu utaokoka. Maana kwa moyo mtu uamini hata kupata haki; na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*" Tunakiri nini? Kwamba tunaamini Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.

  Kumbuka kwamba andiko hilo hapo juu linasema kwamba imani (kuamini), kutubu, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" humanisha kuelekea kitu fulani; sio kwamba tayari umeshakipata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa kuitimiza haki yote, "*Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia, kubali hivi sasa, kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimisha haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye.*" (Mat. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni kitu chema kufanya. Unaona jinsi ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema,

"*imekuwa **kwetu sisi** kuitimiza haki yote.*" Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki Yake, sio kwa sababu ya haki yetu.

Hakika, tusipo batizwa bado tungali katika dhambi zetu. "*Petro, akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" (Mdo. 2:38). Petro, ulisema kusudi la ubatizo ni nini? "*kwa ajili ya ondoleo la dhambi.*" Kwa nini mtu mwingine anaacha hatua hii muhimu inayoondoa dhambi zetu?

Yesu aliagiza kwamba ili kuufikia wokovu ni lazima tubatizwe. "*Akawaambia, enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka asiyeamini atahukumiwa.*" (Mk. 16:15-16).

Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu kama hiki, "*Basi sasa unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshwe dhambi zako, ukiliitia jina lake.*" (Mdo. 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko. "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*" (Rum. 6:4). Utu wetu wa kale umetufia. "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena,*" (Rum. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu inayotumika kwa damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru kutoka katika dhambi zetu za zamani tunapobatizwa.

Hii haimanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatupeleki mwili makaburini na kuuwekea udongo kidogo juu yake; bali tunauzika.

Kama haujafanyika Mkristo, kwa nini usizingatie leo?